TANGAZO LA SERIKALI NA. 64 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA
KATIKA ENEO LA BITIMANYANGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Bitimanyanga ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB1 yenye majira-nukta 547312.84MS, 9173578.05KZ; baada ya hapo mpaka unelekea Kaskazini-Magharibi

katika uelekeo wa 68º32′33″ kwa umbali wa kilomita 1.85 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB2 yenye majira-nukta 545585.12MS, 9174257.14KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata uelekeo wa 18º16′42″ kwa umbali wa kilomita 1.39 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB3 yenye majira-nukta 545146.98MS, 9175583.64KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 10º01′09″ kwa umbali wa kilomita 2.12 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB4 yenye majira-nukta 545515.70MS,
9177671.84KZ baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini-Mashariki katika uelekeo wa 83º42′58″ kwa umbali wa kilomita 2.32 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB5 yenye majira-nukta 547823.52MS, 9177924.97KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki katika uelekeo wa 23º54′11″ kwa umbali wa kilomita 2.44 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba BB6 yenye majira-nukta 548813.209MS, 9175691.936KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa 35º21′57″ kwa umbali wa kilomita 2.59 hadi Ulipoanzia."

Dodoma,
29th Disemba , 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*